

Na: 20. Msimu wa Kilimo 2017/18 Tathmini ya Kipindi cha Aprili 11-20, 2018 na Matazamio kwa Kipindi cha Aprili 21-30, 2018

Muhtasari


- Hali ya unyevunyevu katika udongo inatarajiwa kuendelea kuongezeka zaidi katika maeneo mengi yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka.
- Vipindi vya hali ya ukavu vinatarajiwa kuharakisha kokomaa kwa mazao kuelekea uvunaji katika maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka.
- Wakulima wanashauriwa kutumia dawa za kuzuia fangas kwenye mimea wanaosababishwa na unyenyevu uliokithiri kwenye udongo.

MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA KIPINDI CHA APRILI 11-20, 2018

Katika kipindi cha siku kumi (dekadi) zilizopita, Aprili 11-20, 2018 migandamizo mikubwa ya hewa iliyoko kaskazini mwa dunia (Azores na Siberia) na kusini mwadunia (St. Helena na Mascarene) iliimarika Ukanda wa mvua (ITCZ) uliendelea kuwepo kati ya maeneo kaskazini na kusini mwa Tanzania. Japo kuwa Joto la bahari katika maeneo ya kusini magharibi mwa bahari ya Hindi lilikuwa la wastani hadi chini kidogo ya wastani na kusababisha uwepo hafifu wa vimbunga baharini joto juu kidogo ya wastani lilikuwepo katika maeneo ya Pwani ya afrika mashariki hali iliyopelekea kuwepo kwa mgandamizo mdogo wa hewa na kuimarisha ukanda wa mvua wa ITCZ na kusababisha mvua katika maeneo mengi ya nchi.

MWENENDO WA MVUA KATIKA KIPINDI CHA APRILI 11-20, 2018

Katika kipindi cha dekadhi iliyopita, maeneo mengi ya nchi pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba yalipata mvua za juu ya wastani. Hata hivyo, maeneo machache katika mikoa ya Kagera, Mara, na Kigoma yalipata mvua za wastani kama inavyoonekana kwenye kielelezo hapa chini.



Kielelezo. Kiasi cha mvua (%) kipindi cha tarehe 1-10, Aprili 2018.

TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA APRILI 11-20, 2018

Katika kipindi cha dekadhi iliyopita, maeneo mengi ya nchi yalipata mvua, hali ambayo ilisaidia ukuaji na ustawi wa mazao. Katika maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua mahindi yalikuwa katika hatua ya kubeba na kukomaa hususan katika mikoa ya Iringa, Mbeya, Njombe, Dodoma, Singida, Tabora, Ruvuma, Mtwara na Rukwa. Hata hivyo, baadhi ya maeneno katika mkoa wa Ruvuma (wilaya ya Mbinga) na Mtwara (wilaya ya Newala) mahindi yamekomaa na katika maeneo machache yamekauka wanasubiri kuvuna. Katika mkoa wa Mbeya maharage yapo katika hatua ya kutoa maua, na pia athari za fangas zimeonekana kwenye maharage katika baaadhi ya maeneo ya mkoa wa Mbeya kutokana na unyevunyevu uliokithiri kwenye udongo. Katika maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka, hususan mikoa ya Mara, Kagera, Morogoro na Arusha (wilaya ya Longido) wakulima waliendelea na shughuli za palizi pamoja na upulizaji wa dawa za kuuwa wadudu waharibifu kwa mimea, na mahindi yapo katika hatua ya jani la tatu na jani la tisa. Hata hivyo, imetaarifiwa kuwepo kwa wadudu waharibifu aina ya viwavi jeshi katika maeneo mengi ya mkoa wa Mara, Kilimanjaro, Morogoro (Ilonga) na Manyara (Babati). Pia panya waharibifu wamepungua kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha katika baadhi ya maeneo ya mkoa wa Morogoro. Maharagwe yameharibiwa na mvua nyingi zinazoendelea kunyesha katika Mkoa wa Kagera. Hali ya maji na malisho kwa ajili ya wanyama ilikuwa ya kuridhisha.

HALI YA MAJI ILIVYOKUWA KATIKA KIPINDI CHA APRILI 11-20, 2018

Kina cha maji katika mabwawa, mabonde na mtiririko wa maji katika mito viliendelea kuongezeka hususan katika mabonde ya ziwa Victoria, ziwa Tanganyika, Rukwa, Ruvuma, Rufiji na Nyasa kutokana na mvua zinazoendelea.

**MIFUMO YA HALI YA HEWA
INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA
APRIL 21-30, 2018**

Katika kipindi cha dekadini ijayo, Aprili 21-30, 2018, migandamizo mikubwa iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) inatarajiwa kuendelea kudhoofika wakati ile iliyopo kusini (St. Helena na Mascarene) inatarajiwa kuendelea kuimarika. Ukanda wa mvua (ITCZ) unatarajiwa kuendelea kusogea taratibu kuelekea kaskazini na sehemu kubwa ya nchi inatarajiwa kukaliwa na mgandamizo mkubwa wa hewa hali inayotarajiwa kupunguza mvua. Joto la bahari la wastani hadi chini kidogo ya wastani linatarajiwa katika eneo la kusini magharibi mwa bahari ya Hindi hali inayopunguza uwezekano wa kutokea vimbunga katika bahari. Upepo unatarajiwa kuvuma kutoka mashariki hadi kusini mashariki katika maeneo mengi ya nchi. Eneo la kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola) kunatarajiwa kuwa na joto la bahari la wastani hadi juu kidogo ya wastani. Hali hii itapelekea kupungua kwa upepo uvumao kutoka magharibi hivyo kupunguza mvua katika maeneo ya magharibi mwa nchi.

**HALI YA HEWA INAVYOTARAJIWA KATIKA
KIPINDI CHA APRILI 21-20, 2018**

Kanda ya ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara); Nyanda za juu Kusini magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa) na Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora) inatarajiwa kuwepo na vipindi vya mvua vitakavyo ambatana na ngurumo za radi katika maeneo machache.

Nyanda za juu kaskazini mashariki (Mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro): inatarajiwa kuwepo na vipindi vya mvua katika maeneo machache.

Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba) na pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi) inatarajiwa kuwepo na vipindi vya mvua nyepesi katika maeneo machache.

Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida) na Kanda ya kusini (Mikoa wa Ruvuma na maeneo ya kusini mwa Morogoro) inatarajiwa kuwepo na hali ya ukavu kwa ujumla.

**MATARAJIO NA USHAURI WA KILIMO KATIKA
KIPINDI CHA APRILI 21-30, 2018**

Hali ya unyevunyevu katika udongo inatarajiwa kuendelea kuongezeka zaidi katika maeneo mengi yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka, hali ambayo itasaidia ukuaji na maendeleo ya mazao. Katika maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua, vipindi vya hali ya ukavu vinatarajiwa kuharakisha kokomaa kwa mazao kuelekea uvunaji katika mikoa ya Dodoma, Singida, Ruvuma na maeneo ya kusini mwa Morogoro. Kutokana na kuwepo unyevunyevu uliokithiri katika udongo umepelekea kuwepo kwa madhara ya fangas kwenye mimea, hivyo wakulima wanashauriwa kutumia dawa za kuzuia fangas kwenye mimea. Hali ya maji pamoja na malisho vinatarajiwa kuimarika nchi nzima. Hivyo, wakulima, wavuvi na wafugaji wanashauriwa kuwasiliana na maafisa ugani kwa matumizi sahihi ya utabiri huu.

**HALI YA MAJI INAVYOTARAJIWA KATIKA
KIPINDI CHA APRILI 21-30, 2018**

Kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito vinatarajiwa kuongezeka katika maeneo mengi ya nchi kutokana na mvua zinazotarajiwa. Wananchi wanashauriwa kuimarisha miundombinu ya uvunaji maji ya mvua na kuendelea kuyatumia kwa uangalifu.

Jarida lmetayarishwa na: